# ILEMELA YETU

**Jarida la Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela**

TOLEO MAALUM UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA

**HALIUZWI**

## UJENZI WA VYUMBA 110 VYA MADARASA KWA SHULE 23 ZA SEKONDARI WAKAMILIKA

- Tshs. Bilioni 2.2 fedha kutoka Serikali Kuu zakamilisha ujenzi
- Seti ya viti na meza 5,500 zatengenezwa
- Wanafunzi 12,548 watarajiwa kujiunga kidato cha kwanza 2023



**Eng: Modest Apolinary, Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela amekabidhi vyumba 110 vya madarasa , seti 5500 za meza na viti kwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza mara baada ya ujenzi kukamilika kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza 2023**

*Ilemela ni yetu, Tushirikiane kuijenga*

# TAHARIRI

Sera ya Elimu na mafunzo ya mwaka 2014 inalenga kuwa na mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia ambapo serikali inatamka katika kifungu 3.2.12. kuwa itahakikisha kuwepo kwa miundombinu bora na stahiki ya kutosheleza mahitaji ya elimu na mafunzo kwa makundi yote katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

Kwa kuzingatia sera hii na kutokana na ongezeko la wanafunzi wanaotarajia kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2023 kuwa kubwa ukilinganisha na nafasi zilizoachwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan** aliridhia kutoa kiasi cha shilingi bilioni 160 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 8,000 vitakavyoweza kutosheleza kupokea wanafunzi zaidi ya 400,000 kwa nchi nzima

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ni miongoni mwa halmashauri nufaika ambapo ilipokea kiasi cha Tsh 2,200,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 110 na seti ya meza na viti 5,500 kutoka Serikali Kuu, Fedha hizi ziliingia katika akaunti za shule 23 tarehe 01/10/2022.

Lengo la mradi huu ni kuwezesha wanafunzi wote liochaguliwa kuingia kidato cha kwanza 2023 kupata nafasi na kuanza masomo kwa wakati, pia kuwa na mazingira bora ya kujifunzia na kufundishia.

Mahitaji ya madarasa kwa kidato cha kwanza kwa mwaka 2023 ni vyumba vya madarasa 252 kwa ajili ya wanafunzi 12,548 wasichana wakiwa 6537 na wavulana 6011, vyumba vilivyokuwepo ni 142 na upungufu ulikuwa ni madarasa 110. Hivyo kwa mradi huu wa vyumba 110 utakidhi mahitaji ya wanafunzi wote waliofaulu na kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 11.45 ukilinganisha na mwaka 2021 ambapo wanafunzi 9968 walijiunga na kidato cha kwanza

Hadi kufikia tarehe 21/12/2022 Shule zote zilizopokea fedha zilikamilisha ujenzi wa vyumba 110 vya madarasa vyenye seti ya viti na meza 5,500 na ofisi 3.

Uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela inatoa shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi **Mhe Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Miundombinu ya madarasa kwa wanafunzi watakaojiunga kidato cha kwanza mwaka wa masomo 2023

# Yaliyomo


01 Mkuu Wa Mkoa Wa Mwanza Aipongeza Ilemela Ukamilishaji Wa Vyumba Vya Madarasa

03 Ilemela Wamshukuru Mhe. Rais Ujenzi Wa Vyumba 110 Vya Madarasa

05-28 Picha Za Vyumba 110 Vya Madarasa Katika Shule 23 Za Sekondari Manispaa Ya Ilemela

29 Matukio Katika Picha Makabidhiano Ya Vyumba 110 vya Madarasa

# MKUU WA MKOA WA MWANZA AIPONGEZA ILEMELA UKAMILISHAJI WA VYUMBA VYA MADARASA



*Picha na Habari Na Violeancea Mbakile*

Mhe Adam Malima Mkuu wa Mkoa wa Mwanza ameipongeza Manispaa ya Ilemela kwa ukamilishaji wa vyumba 110 vya madarasa vikiwa na seti 5500 za meza na viti kwa gharama ya kiasi cha Shilingi bilioni mbili na milioni mia mbili fedha iliyotolewa na serikali kuu.

Mhe. Malima ametoa pongezi hizo wakati wa hafla fupi ya makabidhiano ya vyumba vya madarasa hayo mara baada ya ujenzi kukamilika huku akihimiza suala la ukamilishaji wa vyumba vya madarasa ambavyo vimejengwa kwa nguvu za wananchi wa Ilemela ili kuweza kuwatendea haki wanafunzi ambapo ametumia fursa hiyo kuwashukuru na kuwapongeza wananchi wa Ilemela kwa kujenga madarasa 130.

"Katika wilaya zote za Mkoa wa Mwanza, Ilemela mmewapita wote, kwa hili naomba niwapongeze sana lakini naomba nirejee kama tunakuja kupongezana kwa madarasa haya mapya na hatutengi kwenye bajeti zetu marekebisho ya madarasa ya zamani tutakuwa hatutendi haki kwa wanafunzi wanaosoma katika madarasa hayo kwani bila madarasa yale tusingekuwa na haya madarasa 110, amesema Mhe Malima

Pamoja na hayo ameutaka uongozi wa Ilemela kuanza kufikiria suala la matumizi bora ya ardhi kwa kuanza kujenga majengo ya ghorofa ili kuweza kutunza ardhi na kuhifadhi maeneo ya kuchezea watoto na kusisitiza kuwa Mwanza ni mji wa kisasa hivyo mambo yake lazima yaende kisasa.

"Kauli mbiu yangu mimi ni kwamba Mwanza ni mji wa kisasa hivyo lazima mambo yake yawe ya kisasa mnapowaza mambo ya mwanza wazeni kisasa, huko mbele tunapoenda tuanze kufikiria changamoto zinazokuja kwa kufikiria matumizi ya nafasi katika shule zenu kwa maana kuangalia ujenzi wa ghorofa kwa ajili ya kutunza matumizi ya ardhi", amesema Mhe Malima

Ndugu Balandya Elikana, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza akimkaribisha Mkuu wa Mkoa amewataka viongozi na wananchi kwa pamoja kushirikiana na kuhakikisha kuwa wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka 2023 wanaripoti shule mara ifikapo tarehe 09 Januari 2023.

"Ni jukumu kwetu sisi viongozi na wananchi kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa wanajiunga na kidato cha kwanza tushirikiane na tuwahimize vijana wetu kujiunga na kidato cha kwanza na hakuna kitu cha urithi utakachomuachia mtoto isipokuwa elimu na Mhe Rais Dkt Samiah Hassan anafanya kazi kubwa na anaendelea kutoa kipaumbele katika elimu ni muhimu kumuunga mkono kwa kazi kubwa anayofanya lakini tutakuwa tumemuunga mkono kwa kuhakikisha kuwa wote waliochaguliwa kidato cha kwanza wamejiunga, madarasa haya hayatakuwa na maana kama yatabaki matupu hivyo tushirikiane sote kuhakikisha kuwa wanafunzi wanajiunga", amesema Ndugu Balandya

Akisoma taarifa ya makabidhiano Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela Mhandisi Modest Apolinary amebainisha kuwa mahitaji ya madarasa kwa kidato cha kwanza kwa mwaka 2023 ni vyumba vya madarasa 252 kwa ajili ya wanafunzi 12,548 ambapo wasichana ni 6537 na wavulana 6011 , vyumba vilivyokuwepo ni 142 na upungufu ulikuwa ni madarasa 110. Hivyo kupitia kukamilika kwa ujenzi wa vyumba 110 vinaenda utakidhi mahitaji ya wanafunzi wote waliofaulu na kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2023.

Sera ya Elimu na mafunzo ya mwaka 2014 inalenga kuwa na mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia ambapo serikali inatamka katika kifungu 3.2.12. kuwa itahakikisha kuwepo kwa miundombinu bora na stahiki ya kutosheleza mahitaji ya elimu na mafunzo kwa makundi yote katika ngazi zote za elimu na mafunzo.









# ILEMELA WAMSHUKURU MHE. RAIS UJENZI WA VYUMBA 110 VYA MADARASA




*Habari na Picha Na Violeancea Mbakile*

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ni miongoni mwa halmashauri zilizonufaika na fedha kutoka serikali kuu ambapo ilipokea kiasi cha Tsh 2,200,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 110 na seti ya meza na viti 5,500

Kupitia mradi huu wa ujenzi wa vyumba 110 vya madarasa yapo mafanikio mbalimbali ambayo yamepatikana ikiwemo:

- Kupitia Ujenzi wa madarasa haya utasaidia wanafunzi wote waliofaulu na kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza 2023
- Jamii imepata utambuzi namna ya kusimamia miradi ya maendeleo katika maeneo yao
- Kutoa ajira ya muda mfupi kwa wananchi 1412 (Me 1152 Ke 260)
- Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia
- Kuwezesha serikali kupata kodi kutoka kwa mafundi na wazabuni waliouza vifaa

Katika nyakati tofauti wananchi wa Ilemela wameungana kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha hizi:

**Hashim Hussein mzazi wa mwanafunzi maridhia-sekondari ya Kabuhoro** amemshukuru Mhe Rais kwa ujenzi wa madarasa ambapo hapo nyuma wazazi walikuwa wakichangishwa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, na kuongeza kusema kuwa mazingira huchangia kupata moyo wa kusoma kwani hapo awali wanafunzi walikuwa wakisoma kwa shida kutokana na uhaba wa madarasa kwani wanafunzi walikuwa wanabanana darasani hivyo itampa fursa mwalimu kufundisha vizuri. Na kutoa wito kwa wazazi wote kuwahimiza watoto kusoma kwa bidii na walimu wafanye juhudi ya kufundisha ili kuboresha elimu zaidi "Tunamshukuru Mhe Rais kuboresha elimu kwani elim u ndio jambo la kwanza kabla ya yote", amesema Ndugu Hussein

**Tabia Protatius**:Amempongeza Rais kwa hatua hii ya ujenzi wa madarasa kwani ni jambo ambalo amekuwa akilifikiria muda mrefu kutokana na kuwa hapo awali kulikuwa na mbanano katika madarasa

**Evarist Sungura:** amesema kuwa hapo awali alipokuwa mwenyekiti wa kamati ya ujenzi na walipendekeza kuchangisha wazazi kiasi cha shilingi elfu 10 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kulikuwa na changamoto ya wazazi kutoa fedha fedha hizi zimeleta unafuu sana kwa wazazi, hivyo amemshukuru Mhe Rais kwa hilo

**Neema Albert mzazi wa mwanafunzi shule ya Angeline Mabula** yeye amemshukuru Mhe.

Rais kwa kuwapunguzia gharama za kuchangia fedha za ujenzi wa madarasa pamoja na meza na viti, pamoja na hilo amemshukuru Rais kwa kuondoa ada kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita amefarijika kwani watoto watasoma kwa uhuru

**Fatma Abdalah Akilimali -mkuu wa shule kabuhoro:** Hapo awali wazazi walikuwa wanachangishwa na kuambiwa waje na meza na viti tofauti na sasa kwani kila kitu kipo ni jukumu la mzazi kuhakikisha wanafunzi wote wanaripoti shule mwaka 2023

**Majaliwa Gerana mkuu wa shule Angeline Mabula:** Amemshukuru Mhe Rais kwani madarasa haya yanaenda kupunguza msongamano mkubwa madarasani na wanafunzi wanaenda kusoma katika mazingira mazuri na hivyo kuboresha hali ya ufaulu

**Matono-fundi wa meza na viti**: Amemshukuru mhe Rais kwa fedha za ujenzi wa madarasa kwani kupitia mradi huu wameweza kunufaika na miradi mbalimbali ambapo kwa upande wake ameweza kutengeneza meza na viti katika shule tatu ambapo ameweza kutengeneza meza na viti 900 kutokana na fedha hizo amenufaika kwa namna ya uendeshaji wa ofisi kukuza jina la biashara pamoja na hilo ameweza kuajiri vijana mbalimbali takriban 20 wauza mbao, pamoja na vifaa mbalimbali vya matengenezo huku akiomba jamii kuendelea kushirikishwa katika miradi mbalimbali

**Ibrahim Bahati Mussa Fundi rangi**: Amemshukuru Mhe Rais kwa mafundi ambao ni local fundi wameweza kupata fursa hii ambapo ameweza kuajiri na vijana wengine shukrani kwa mhe Rais kwa kutambua uwepo wa mafundi ambao sio Wahandisi wameweza kuajiriwa wazawa wa eneo husika.

**Catherine Ayubu-Mkazi wa Buswelu**: Kibarua katika kazi ya utengenezaji wa meza na viti akisugua msasa fedha anayoipata anaitumia kwa matumizi yake mbalimbali kama kuwanunulia wajukuu zake mahitaji ya shule anamshukuru Rais wamepata ajira kupitia ujenzi huu na pia shule zinaenda kupendeza

**Lulu Martin- Kidato Cha Tatu Kabuhoro Sec**
Yeye anamshukuru Mhe Rais na kukumbuka wakati anaripoti mwaka 2020 hali ya madarasa haikuwa nzuri kwani waliambiwa kuripoti wakiwa na meza na viti, lakini kwa sasa madarasa yanapendeza yakiwa na vigae, madirisha mazuri na meza na viti wanafurahia hali hiyo wakiamini wadogo zao wa kidato cha kwanza watakapo ripoti shule watakutana na mazingira mazuri hivyo kuchochea ufaulu amemuomba Mhe Rais mradi huu kuendelea hivi ili kuwawezesha wanafunzi kusoma vizuri na kuchochea ufaulu

**Leticia Martin Kidato Cha Kwanza (2022) Angeline Mabula**
Ameshukuru kwa fedha za ujenzi wa madarasa hata aliporipoti kidato cha kwanza mwaka 2022 walikuta madarasa mazuri na meza na viti na hivyo kupunguza gharama kwa wazazi na kwasasa wanaona ujenzi wa madarasa mengine katika shule yao ambapo itawasaidia wanafunzi wa kidato cha kwanza kusoma vizuri huku akimuahidi Mhe. Rais kusoma kwa bidi ili kutimiza lengo lake la kuwa rubani wa ndege.

**Latifa Ramadhan Salum Kidato Cha Kwanza 2022 Angeline Mabula**
Yeye anasema wakati anaripoti kidato cha kwanza mwaka 2022 walikuta mazingira ya shule mazuri na hawakuambiwa kuleta meza wala viti madarasa yana muonekano mzuri ambao unasaidia hata kipindi cha mvua kwani madarasa yana vioo, hayavuji hivyo kumuwezesha mwanafunzi kusoma vizuri na kumpa motisha ili aweze kufaulu Pamoja na hilo amemshukuru Mhe. Rais kwa kuondoa ada na kuendeleza miradi ya shule

**Brian John Nkyalu Kidato Cha Tatu Angeline Mabula**
Muonekano mzuri wa madarasa unasaidia kukuza taaluma ya mwanafunzi, madarasa yamekuwa msaada mkubwa kwa wazazi wao kwani tayari madarasa yana kila kitu na ni imara tofauti na hali ya zamani ilikuwa ukiripoti lazima uje na meza na viti lakini kwa sasa changamoto hiyo imeondolewa ameishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan

**Zakaria Ngumije Mwanafunzi Kabuhoro Sekondari**
Ameishukuru serikali ya Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha shule yake ya Kabuhoro ujenzi wa vyumba vitano vya madarasa Pamoja na hilo ameushukuru uongozi wa shule na viongozi wa mtaa kwa kuhakikisha kuwa mradi huu unakamilika ili kuwezesha wadogo zao watakaoripoti kidato cha kwanza 2023 watakuta mazingira ya kujifunzia ni mazuri hivyo kusababisha kuongezeka kwa ufaulu.

# SHULE YA SEKONDARI YA ANGELINE MABULA
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 120
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: SITA
# SETI YA VITI NA MEZA : 300











SHULE YA SEKONDARI YA BUGOGWA
KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 200
IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: KUMI
SETI YA VITI NA MEZA : 500











# SHULE YA SEKONDARI YA BUJINGWA
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 160
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: NANE
# SETI YA VITI NA MEZA : 400











# SHULE YA SEKONDARI YA BUSWELU
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 160
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: NANE
# SETI YA VITI NA MEZA : 400











# SHULE YA SEKONDARI YA BUZURUGA
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 280
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: 14
# SETI YA VITI NA MEZA : 700











# SHULE YA SEKONDARI YA IBINZA
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 140
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: SABA
# SETI YA VITI NA MEZA :350











# SHULE YA SEKONDARI YA IBUNGILO
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 80
# IDADIYAVYUMBAVYAMADARASA:MANNE
# SETI YA VITI NA MEZA : 200











# SHULE YA SEKONDARI YA IGOGWE
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 20
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: MOJA
# SETI YA VITI NA MEZA : 50











# SHULE YA SEKONDARI YA KABUHORO
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 100
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA:MATANO
# SETI YA VITI NA MEZA : 250













# SHULE YA SEKONDARI YA KANGAYE
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 120
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: SITA
# SETI YA VITI NA MEZA : 300











# SHULE YA SEKONDARI YA KAYENZE
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 100
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: MAWILI
# SETI YA VITI NA MEZA : 100











# SHULE YA SEKONDARI YA KILIMANI
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 60
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: MATATU
# SETI YA VITI NA MEZA : 150











# SHULE YA SEKONDARI YA KIRUMBA
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 20
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA:MOJA
# SETI YA VITI NA MEZA : 50











# SHULE YA SEKONDARI YA KISUNDI
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 40
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: MAWILI
# SETI YA VITI NA MEZA : 100











# SHULE YA SEKONDARI YA KITANGIRI
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 100
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: MATANO
# SETI YA VITI NA MEZA : 250











# SHULE YA SEKONDARI YA LUKOBE
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 80
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: MANNE
# SETI YA VITI NA MEZA : 200











# SHULE YA SEKONDARI YA LUMALA
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 40
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: MAWILI
# SETI YA VITI NA MEZA : 100











# SHULE YA SEKONDARI YA MWINUKO
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 20
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: MOJA
# SETI YA VITI NA MEZA : 50











# SHULE YA SEKONDARI YA NUNDU
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 40
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: MAWILI
# SETI YA VITI NA MEZA : 100











# SHULE YA SEKONDARI YA NYAMANORO
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 20
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: MOJA
# SETI YA VITI NA MEZA : 50











# SHULE YA SEKONDARI YA NYAMHONGOLO
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 120
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: SITA
# SETI YA VITI NA MEZA : 300











# SHULE YA SEKONDARI YA SEMBA B
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 60
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA:MATATU
# SETI YA VITI NA MEZA : 150











# SHULE YA SEKONDARI YA SHIBULA
# KIASI CHA FEDHA: SHILINGI MILIONI 180
# IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA: 9
# SETI YA VITI NA MEZA : 450









# MATUKIO KATIKA PICHA MAKABIDHIANO YA

# VYUMBA 110 VYA MADARASA



Eng.Modest Apolinary(Mkurugenzi wa Manispaa akisoma taarifa ya makabidhiano ya vyumba 110 vya madaarasa



Mhe. Adam Malima(RC-MWANZA) akikata utepe kuashiria kukamilika kwa ujenzi wa vyumba 110 vya madarasa Manispaa ya Ilemela



Wakuu wa Shule za Sekondari Manispaa ya Ilemela wakifuatilia tukio zima la makabidhiano ya vyumba 110 vya madarasa



Mkuu wa Mkoa akikagua kishkwambi kabla ya kuvikabidhi kwa walimu wa shule za Msingi na Sekondari, maafisa Elimu Ngazi ya Kata na Maafisa Elimu Wilaya



Mhe Adam Malima (RC) akikagua ubora wa meza na viti katika moja ya darasa shule ya sekondari Bujingwa



Mhe. Adam Malima(RC-Mwanza), na Mhe. Hassana Masala(DC-Ilemela) Wakiteta jambo wakati wa hafla ya makabidhiano ya madarasa

# HALIUZWI

**Jarida hili Limeandaliwa na:**

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela

SCAN HAPA KUPERUZI
TOVUTI YA ILEMELA

OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA
200BR.YA BUSWELU
33282 BUSWELU
ILEMELA,MWANZA

Tufuatilie >>> ilemelamamc | www.ilemelamc.go.tz
Barua Pepe: md@ilemelamc.go.tz